# TANGAZO

**MAELEKEZO KUHUSU UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2019 KWA WANANCHI WA HALMASHAURI YA MJI MASASI**

**TAREHE 23/09/2019**

Kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Miji za Mwaka 2019 kifungu 9 (1) (2) na Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji za Mwaka 2019 kifungu 9 (1) (2), Msimamizi wa Uchaguzi anatoa maelekezo yafuatayo kwa wananchi wote wa Halmashauri ya Mji Masasi kuhusiana na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019

1. Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utafanyika tarehe 24/11/2019 siku ya Jumapili ambapo, katika eneo la Mjini lina jumla ya Kata 8 ambazo ni Chanikanguo, Mtandi, Jida, Napupa, Mkuti, Migongo, Nyasa na Mkomaindo hivyo kutakuwa na vituo vya kupigia kura 57 na nafasi zifuatazo kugombewa kwa kila Mtaa;

- Mwenyekiti wa Mtaa
- Wajumbe Viti Maalum 2 na
- Wajumbe Mchanganyiko 3

Kwa eneo ambalo lina Kata za Mumbaka, Mwengemtapika, Matawale, Sululu, Temeke na Marika lina jumla ya vijiji 31

ambapo kutakuwa na vituo 149. Nafasi zifuatazo zitagombewa

- Mwenyekiti wa Kijiji
- Mwenyekiti wa Kitongoji (kutegemea na idadi ya vitongoji katika kijiji)
- Wajumbe Viti Maalum (wasiozidi 8) watakaounda Halmashauri ya Kijiji na
- Wajumbe Mchanganyiko (kwa nafasi zinazobaki kufanya idadi ya wajumbe 25 ya Halmashauri ya kijiji)

2. Uandikishaji wa Wapiga Kura utafanyika kwa muda wa siku saba kuanzia tarehe 08/10/2019 hadi 14/10/2019. Zoezi hili litafanyika katika majengo ya umma (Shule, Ofisi za Serikali kama vile majengo ya AMCOS, Zahanati, Ofisi za Vijiji na Kata) na maeneo mengine ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa amekubaliana na Viongozi wa Vyama vya Siasa kwa eneo ambalo hakuna jengo la Serikali. Uandikishaji utafanyika kuanzia **saa mbili (2) asubuhi hadi saa kumi na mbili (12) jioni**. Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa, Wajumbe Viti Maalum na Wajumbe mchanganyiko utafanyika katika Mtaa husika na Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kitongoji, Wajumbe Viti Maalum na Wajumbe mchanganyiko utafanyika katika vitongoji vilivyomo katika Kijiji

3. Wapiga kura wanatakiwa wawe na sifa zifuatazo:
   i. Ni raia wa Tanzania

ii. Wenye umri kuanzia miaka 18 au zaidi
iii. Awe mkazi wa Mtaa/Kitongoji husika
iv. Awe hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu
v. Awe amejiandikisha kupiga kura katika Mtaa/Kitongoji husika

4. Wagombea Uongozi wanatakiwa wawe na sifa zifuatazo:
   i. Ni raia waTanzania
   ii. Wenye umri wa miaka 21 au zaidi
   iii. Wenye uwezo wa kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza
   iv. Awe na shughuli halali ya kumuwezesha kuishi
   v. Awe ni mkazi wa Mtaa/Kitongoji husika
   vi. Awe mwanachama wa Chama cha siasa na awe amedhaminiwa na chama hicho
   vii. Awe hajawahi kupatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu katika **kipindi cha miaka 5** kabla ya tarehe ya Uchaguzi
   viii. Awe hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu.

5. Fomu za kugombea Uenyekiti wa Mtaa, Wajumbe Viti Maalum wa Mtaa na Wajumbe Mchanganyiko wa Mtaa katika maeneo yenye Mitaa na fomu za kugombea Uenyekiti wa Kijiji, Uenyekiti wa Kitongoji, Wajumbe Viti Maalum na Wajumbe Mchanganyiko kwenye maeneo

yenye Vijiji zitatolewa kuanzia tarehe 29/10/2019 hadi 04/11/2019 na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wa eneo husika. Uchukuaji na urejeshaji wa fomu hizo hautazidi siku saba na tarehe 04/11/2019 saa **kumi jioni** itakuwa siku ya mwisho ya kurejesha fomu.

6. Uteuzi wa wagombea kwa nafasi zote zinazogombewa utafanywa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi tarehe 5/11/2019 kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi jioni. Pia Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atabandika fomu za wagombea walio na sifa na wasio na sifa mahali pa matangazo ya uchaguzi

7. Mgombea au Mtu aliyeomba kuteuliwa kuwa mgombea anaweza kuweka pingamizi dhidi ya uteuzi wa Mgombea au wagombea kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi tarehe 05-6/11/2019. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atasikiliza na kutoa uamuzi katika muda usiozidi siku mbili tangu kupokelewa kwa pingamizi hilo.

8. Mgombea au Mtu aliyeomba kuteuliwa kuwa mgombea asiporidhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa na haki ya kukata rufaa kwenye Kamati ya Rufaa kwa muda usiozidi siku nne (4) kuanzia tarehe 05/11/2019 hadi 08/11/2019.

9. Kamati ya rufaa itashughulikia rufaa ya Mgombea au Mtu aliyeomba kuteuliwa kuwa mgombea dhidi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi. Kamati itatoa uamuzi wa rufaa

ndani ya muda wa siku nne kuanzia siku ya kupokea rufaa yaani 05-09/11/2019. Ambaye hataridhika na uamuzi wa Kamati ya rufaa anaruhusiwa kufungua shauri katika Mahakama ya Wilaya ndani ya siku 30 baada ya matokeo ya Uchaguzi kutangazwa

10. Mikutano ya kampeni za Uchaguzi itafanyika kwa siku saba (7) za mwisho kabla ya siku ya uchaguzi na zitamalizika siku moja kabla ya siku ya Uchaguzi yaani kuanzia tarehe 17/11/2019 hadi 23/11/2019. Mikutano ya kampeni itafanyika kuanzia saa **mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni**

11. Msimamizi wa Kituo anaweza kumtaka Mpiga Kura kuonesha kitambulisho kitakachoonesha kuwa jina la mpiga kura huyo ndilo lililomo kwenye Orodha ya Wapiga Kura. Vitambulisho hivyo vinaweza kuwa;
    - Kitambulisho cha kupigia kura
    - Kitambulisho cha Kazi
    - Kadi ya Bima ya Afya
    - Kitambulisho cha Shule/Chuo
    - Kitambulisho cha Hifadhi ya Jamii
    - Leseni ya Udereva
    - Kitambulisho cha Utaifa
    - Kama hana kitambulisho basi aweze kutambuliwa na Wakazi wa eneo husika

12. Wananchi wote wenye sifa mnashauriwa kujitokeza kwa wingi na kujiandikisha ndani ya tarehe zilizopangwa na tarehe ya kupiga kura itakapofika wote nendeni mkapige kura.

Tangazo hili limetolewa na:

**Zuena Ungele**
**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI**
**HALMASHAURI YA MJI MASASI**